# JINSI YA KUHAKIKISHA MTEJA SI MJAMZITO

*Orodha ya Jinsi ya Kuhakikisha Mteja si Mjamzito* ni kitendea kazi cha wahudumu wa afya cha kuthibitisha kwamba mwanamke anayetaka kuanza kutumia njia ya mpango wa uzazi **SI** mjamzito. Orodha hii imebuniwa ili itumiwe na wahudumu wa afya wa viwango vyote vya utoaji wa huduma za mpango wa uzazi nchini Kenya, ikiwa ni pamoja na wahudumu wanaotoa huduma za utibabu (madaktari, manesi na wakunga) na wale wasiotoa huduma za utibabu (wafanyikazi wa afya ya jamii na famasia).

Wizara ya Afya, tawi la afya ya uzazi (DRH) ikishiriakiana na Family Health International, imetengeneza orodha hii kwa matumizi wakati wa kutathmini hali ya afya ya wateja kabla ya utoaji huduma za mpango wa uzazi kama ilivyoelezwa katika vigezo vya taratibu za kutoa huduma hizo *(Kenya Family Planning Guidelines for Service Providers - March 2005)*. Kwa mujibu wa vigezo hivi, wahudumu wa mpango wa uzazi wanalazimika kuthibitisha ikiwa mwanamke anayetaka kutumia njia ya mpango wa uzazi huenda tayari ana mimba. Hii ni kwa sababu wanawake ambao ni wajawazito hawahitaji kuzuia mimba. Zaidi ya hayo, njia za uzuiaji mimba kama vile *"kitanzi" (Copper IUD)* hazitakiwi kabisa kutumika na wanawake wajawazito kwani zikitumiwa zinaweza kusababisha tatizo lenye hatari, kama kutokwa kwa mimba iliyopata bakteria. Iwapo nyenzo za kimaabara za upimaji mimba hazipo ua wateja hawawezi kuzilipia, wateja wanahitajika kungojea kupata hedhi (damu ya mwezi) kabla ya kupata huduma za mpango wa uzazi. Hii ni kwa sababu wahudumu hutegemea kuweko kwa damu hii kama kiashiria kuwa mwanamke si mjamzito. Orodha hii imetengenezwa kukabili tatizo hili la uhaba wa nyenzo za kimaabara. Orodha hii ina maswali sita (6) yaliyoidhinishwa na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) kubainisha kwa uhakika kwamba kweli mwanamke si mjamzito. Tathmini ya orodha hii katika vituo vya upangaji uzazi Kenya imehakikisha kuwa nyenzo hii ina uwezo mwafaka wa kutambua kwa usahihi wanawake ambao si wajawazito. Zaidi ya hayo, utafiti wa hivi karibuni nchini Guatemala, Mali, na Senegal umeonyesha kuwa utumiaji wa orodha hii ya kupimia na wahudumu wa kupanga uzazi imepunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya wateja wanaokosa kupata huduma za uzuiaji mimba kwa ajili ya hali zao za hedhi.

Orodha hii ni mojawapo ya mfuatano wa orodha za kupimia zilizotengenezewa wahudumu wa mpango wa uzazi Kenya. Orodha nyingine za kupimia ni pamoja na *Orodha ya kuthibitisha wateja wanaotaka kuanzisha utumiaji wa tembe changamano za kuzuia mimba (COCs), Orodha ya kuthibitisha wateja wanaotaka kuanzisha utumiaji wa DMPA (au NET-EN), na Orodha ya kuthibitisha wateja wanaotaka kuanzisha utumiaji wa kitanzi (Copper IUD)*. Kwa maelezo zaidi kuhusu orodha za kupimia za mhudumu, tembelea mtandao wa Wizara ya Afya Kenya www.drh.go.ke.

## Maelezo ya Maswali

Orodha hii ina maswali sita ambayo wahudumu huwauliza wateja wanapochukua historia yao ya kimatibabu. Iwapo mteja atajibu 'NDIO' kwa swali lolote lile, na hana dalili au ishara yoyote ya kuwa na mimba, basi mhudumu anaweza kuwa na uhakika kwamba mwanamke huyo hana mimba.

Wanawake walio kwenye siku saba za kwanza ya mzunguko wa hedhi yao, waliopata kutokwa mimba katika siku saba zilizopita, au walio kwenye majuma manne ya mwanzo baada ya kujifungua, wamelindwa na kupata mimba isiyokuwa imepangwa kwa sababu uwezekano wa kupata mimba katika hali hizo ni mdogo sana. Kwa utumiaji wa Kitanzi (Copper IUD), uwezekano wa kupata mimba ni mdogo sana kabla ya siku ya kumi na mbili (12) katika mzunguko wa hedhi kwa sababu ya uwezo mwafaka wa Kitanzi (Copper IUD) kuzuia mimba. Wanawake wanaotosheleza kigezo cha njia ya *'Lactational Amenorrhea Method'* (wanawake walio katika miezi sita ya kwanza baada ya kujifungua, wanaonyonyesha maziwa ya mama pekee, na damu yao ya hedhi bado haijarudi) wamelindwa kupata mimba isiyokuwa imepangwa kwa sababu ya athari za kukosa hedhi wakati wa *"Lactational Amenorrhea"* kwenye mzunguko wa uzazi. Kadhalika, wanawake wanaotumia njia ya kuaminika ya kupanga uzazi kama inavyotakiwa wamekingwa vilivyo kutokana na mimba, hali kadhalika, wale ambao wamejinyima ngono tangu hedhi yao ya mwisho.

## Asili:


1. Technical Guidance/Competence Working Group (TG/CWG). *Recommendations for Updating Selected Practices in Contraceptive Use: Volume II.* Washington: U.S. Agency for International Development, 1997.
2. Stanback J, Qureshi Z, Nutley T, Sekadde-Kigondu C. Checklist for ruling out pregnancy among family-planning clients in primary care. *Lancet* 1999;354(August 14):566.
3. Stanback, John, Diabate Fatimata, Dieng Thierno, Duarter de Morales, Cummings Stirling, and Traore Mahamadou. Ruling Out Pregnancy Among Family Planning Clients: The Impact of a Checklist in Three Countries. *Studies in Family Planning* 2005;36[4]:311–315.



Republic of Kenya

**Kenya 2008**

# JINSI YA KUHAKIKISHA MTEJA SI MJAMZITO

Muulize mteja maswali 1-6. Mara tu anapojibu NDIO kwa swali lolote lile, usiendelee kumuuliza maswali yanayofuata, na fuata maagizo ya orodha hii.

| | | | |
|---|---|---|---|
| LA | 1. | Je, ulijifungua mtoto chini ya miezi 6 iliyopita, unamnyonyesha maziwa ya mama pekee, na hujapata damu ya mwezi tangu ujifungue? | NDIO |
| LA | 2. | Je, umejinyima ngono tangu upate damu yako ya mwezi ya mwisho au kuzaa? | NDIO |
| LA | 3. | Umepata mtoto katika majuma manne (4) yaliyopita? | NDIO |
| LA | 4. | Je, damu yako ya mwezi ilianza kwenye siku saba (7) zilizopita (au kwenye siku kumi na mbili (12) zilizopita ikiwa unapanga kutumia kitanzi)? | NDIO |
| LA | 5. | Je, umetokwa na mimba katika siku saba (7) zilizopita? (ua siku kumi na mbili (12) zilizopita ikiwa unapanga kutumia kitanzi)? | NDIO |
| LA | 6. | Je, umekuwa ukitumia njia ya kuzuia mimba inayoaminika kila wakati na vile vile kama inavyotakikana? | NDIO |

Ikiwa mteja alijibu **LA** kwa ***maswali yote***, mhudumu hawezi kuwa na uhakika kwamba mwanamke si mjamzito. Mteja anatakiwa angojee apate damu ya hedhi au apimwe mimba kutumia kigezo cha kimaabara.

Ikiwa mteja alijibu **NDIO** kwa angalau ***swali moja*** na hana dalili au ishara za mimba, mpatie mteja dawa ya kuzuia mimba anayotaka.

Republic of Kenya

Division of Reproductive Health, Kenya Ministry of Health, Old Mbagathi Road, P.O. Box 43319-00100, Nairobi, Kenya
Telephone: 254-020-2725105 Fax: 254-020-2716814
Website: www.drh.go.ke